# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO

## Jarida la Robo ya Tatu ya Mwaka

## (Januari - Machi)

**Toleo Na. 0003**
**04, Aprili 2023**



**Tufuatilie:**

Chamwino Dc

Chamwino_dc

www.chamwinodc.go.tz

1126 Chamwino, Dodoma, Tanzania

#KAZI IENDELEE

# Yaliyomo

3 Naibu Waziri Ndejembi Akabidhi Vifaa Vya Ujenzi, Chamwino

4 Chamwino Yaungana na Wanawake Mkoa wa Dodoma Kuazimisha Siku ya Wanawake Duniani

6 Chuo Kikuu cha UDOM Watoa msaada Shule ya Msingi Buigiri Blind

8 Wadau wa Elimu Chamwino Waweka Maadhimio Kuboresha Elimu

10 Mafunzo ugawaji wa Neti Mashuleni

12 Chamwino Yapongezwa Ukusanyaji Wa Mapato

BODI YA WAHARIRI
Modesta Simon

# Naibu Waziri Ndejembi Akabidhi Vifaa Vya Ujenzi, Chamwino



Naibu Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Deogratius Ndejembi amekabidhi mifuko ya simenti na mabati kwa ajili utekelezaji wa miradi kwa jimbo la Chamwino leo, Machi 10, 2023. Makabidhiano yamefanyika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino.

Akikabidhi vifaa hivyo Mhe. Waziri amewataka waheshimiwa Madiwani na wataalam wote waliokabidhiwa vifaa hivyo kuhakikisha vinafanya kazi ya miradi iliyokusudiwa na inakamilika kwa wakati.

" Kubwa ambalo nasisitiza ni usimamizi wa vitendea kazi hivi viweze kutumika kama malengo yanavyotaka na mkiacha usimamizi ni kumaliza miradi kwa wakati na hii si tu kwa waheshimiwa Madiwani bali hata watumishi kwa ujumla".

" Changamoto kubwa tuliyonayo Serikali za Mitaa ni miradi ya Serikali kutokamilika kwa wakati lakini si tu kukamilika kwa wakati baki hata usimamizi waje huwa duni na ndio unakuta miradi inachelewa. Na hizi fedha zinaletwa na Mhe. Rais wetu Samia Suluhu Hassan ili zije kuhudumia wananchi na si kutuhudumia sisi viongozi."

Jumla yamifuko 1950 ya simenti na mabati 130 yamegawiwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo 30.

Alimshukuru Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kumuamini na kumteuwa kuwa Naibu Waziri wa TAMISEMI na àliahidi kufanya kazi kwa bidii kama matarajio Ya Mhe. Rais

Naye Diwani wa Kata ya Buigiri ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe. Keneth Yindi alimshukuru Mhe. Naibu Waziri kutokana na mtumizi yaliyowazi kwa fedha za Mfuko wa Jimbo kwani vifaa hivyo vimegawiwa mbele ya Waheshimiwa Madiwani wote kwa kadri ya mahitaji yao waliyoyawasilisha.

" Mhe. Naibu Waziri wa TAMISEMI kwa niaba ya Halmashauri nashukuru kwa matumizi yaliyowazi ya fedha za mfuko wa jimbo.umeona suala hili liwe la wazi umewaita Madiwani wote na kila Diwani amepata kulingana na mahitaji yake na hii inaonyesha sisi ni wamoja na angeomba iwe mfano kwa maeneo mengine katika kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi."



# Chamwino Yaungana na Wanawake Mkoa wa Dodoma Kuazimisha Siku ya Wanawake Duniani




Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imeungana na Taasis nyingine Mkoani Dodoma kuazimisha siku ya Wanawake Duniani ambayo hufanyika Machi 8 ya kila mwaka.

Kwa mkoa wa Dodoma maadhimisho haya yalifanyika kimkoa Wilaya ya Kondoa viwanja vya sabasaba na kuhudhuriwa na Taasis mbalimbali zilizoko mkoa wa Dodoma, Taasis za Serikali na zisizo za Serikali.

Katika maadhimisho hayo Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imeweza kutoa wanafunzi watatu wa kike waliofanya vizuri kwa kupata daraja A kutoka katika shule za kata za Buigiri ambapo mwanafunzi aliyepata zawadi ni Furaha Bahati Lusulo, Mlowa Barabarani aliyepata zawadi ni Neema Gerad Maiko na Chilonwa ni Maria Julius Maning, pia mwanamke kinara Bibi Joanitha aliweza kupata zawadi.

Vilevile kikundi cha Ujirani mwema kutoka Kata ya Manchari kiliweza kupata zawadi ambazo zilikuwa zinatolewa kwa vikundi bora vya wanawake.

Aidha Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imeshika nafasi ya tatu kwa utoaji wa mikopo kwa vikundi kwa Halmashauri zote za mkoa wa Dodoma na kushika nafasi ya pili kwa Halmashàuri zinazofuatilia marejesho ya mikopo na kurejesha vizuri kwa vikundi vya wanawake, vijana na wenyeulemavu vilivyopatiwa mikopo.

Katika maadhimisho hayo mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa na wanawake mkoa wa Dodoma yalibainishwa. Nawanawake waliaaswa kuhakikisha wanapiga hatua zaidi katika kushika nafasi za uongozi.

Suala la malezi ya watoto halikuachwa nyuma, wazazi walisisitizwa kuwalea watoto katika maadili mema ili kuwaepusha kujiingiza kwenye mambo maovu ya panya road na ushoga na ukatili wa kijinsia yanayoendelea kwenye jamii yetu.

Mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Staki Senyamule na viongozi mbalimbali wa Serikali walihudhuria akiwepo Waziri wa uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Ashantu Kijaji.



# Kuelekea kilele cha Siku ya Wanawake Duniani Chamwino Yaazimisha kwa Kuchangia Nguvu Kazi Ujenzi wa Zahanati



Kuelekea kilele cha Siku ya Wanawake duniani Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imeadhimisha kwa kuchangia nguvu kazi kwenye ujenzi wa zahanati ya kijiji cha Chitàbuli kata ya Membe leo Machi 3, 2023.

Akizungumza katika maadhimisho hayo mgeni rasmi Katibu Tawala wa Wilaya Bi Neema Nyalege aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya Mhe. Gift Isaya Msuya amewapongeza kwa jambo zuri la kuanźisha ujenzi wa zahanati. Alitoa rai waendelee kuhamasishana ili kukamilisha ujenzi huo ili Serikali iweze kukamilisha walau kufikia bajeti ya mwaka ujao wa 2023/2024

Vilevile Elimu imeweza kutolewa ya namna ya kukabiliana na suala zima la ukatili mbalimbali unaotokea kwenye jamii, namna ya kupata msaada wa kisheria, mbinu za kilimo bora hususani suala là kilimo cha mbogamboga





# Chuo Kikuu cha UDOM Watoa msaada Shule ya Msingi Buigiri Blind

Chuo kikuu cha Dodoma (UDOM) kimetoa msaada wa madaftari, kalamu za wino, penseli,Vifutio na biscuit kwa wanafunzi wa shule ya msingi Buigiri Blind.

Msaada huoumetolewa na Prof. Julius Nyahongo, Rais wa Ndaki ya Elimu ambaye alimuwakilisha Makamu Mkuu wa Chuo cha Dodoma.

Makabidhiano hayo yamefanyika Februari 25, 2023 shule ya msingi Buigiri Blind mbele ya viongozi wa Halmashauri akiwemo Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe. Keneth Yindi na mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Bibi Zaina Kishegwe yàkishuhudiwa na viongozi wa Skauti na viongozi wa TPO









# Makabidhiano ya pikipiki

Afisa Utumishi Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino Bi Christina Sam amekabidhi pikipiki kwa watendaji wa kata kwa niabà ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya Dr. Semistatus Mashimba Februari 21, 2023.

Pikipiki hizi zimetolewa na Wizara ya Ofisi ya Rais TAMISEMi kwa ajili ya kurahisha utendaji kazi kwa Watendaji wa kata zilizoko pembezoni.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo Bi Christina amewataka watendaji hao kuhakikisha wanavitunza vyombo hivyo nakuvitumia kwa malengo yaliyokusudiwa na si kwenda kuzigeuza kuwa bodaboda.

" Hakikisheni mnazitunza pikipiki hizi na kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa, msiende kuzigeuza kuwa bodaboda." Alisema Afisa Utumishi.

Halmashauri ilipokea jumla ya pikipiki 9 na zote zimegawiwa kwa kata za Chiboli, Manda, Manzase, Loje, Zajilwa, Haneti, Dabalo, Membe na Ng'hambaku.



# Wadau wa Elimu Chamwino Waweka Maadhimio Kuboresha Elimu

Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imefanya kikao cha wadau wa elimu Wilaya leo Februari 16, 2023, kwa lengo la kufanya tathimini kuona walichopanga na wapi walipofika katika utekelezaji wa malengo waliyojiwekea. Kikao kimefanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Halmashàuri.

Akizungumza alipokuwa akifungua kikao hicho Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Chamwino ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Kongwa Mheshimiwa Remidius Mwema Emmanuel amesema kama Wilaya waangalie mambo yaliyowavuta nyuma ili wayarekebishe.

Aidha Mkuu wa Wilaya alieleza



kuwa Chamwino imedhamiria kuleta mapinduzi makubwa kwenye eliju kwa kuona mabadiliko kwa kila mwaka.

Katika kikao hicho Maafisa Elimu Msingi na Sekondari waliwasilisha taarifa za hali ya Elimu kila mmoja na baada hapo wajumbe walijadili nakuweka maadhimio mbalimbali yatakayoweza kusaidia katika suala la kuboresha hali ya elimu ndani ya Wilaya.

Miongoni mwa madhimio yaliyofikiwa ni pamoja na utoaji wa motisha kwa walimu kuanzia ngazi ya kijiji hadi Wilaya pamoja na maslahi na stahiki za walimu kutolewa kwa wakati.

Kila shule kulima mashamba na kuweka vitega uchumi kwa ajili ya kutoa chakula shuleni.

Walimu wakuu na Wakuu wa shule kupimwa kwa ufaulu shuleni na kutoa bendera nyeusi kwa shule zinazofanya vibaya.

Kutoa Elimu kwa wazazi, wanafunzi na jamii nzima kuhusu umuhimu wa elimu

Ufanyaji wa mazoezi na mitihani ya mara kwa mara kwa wanafunzi pamoja na kuwepo na jitihada za kuondoa alama Dna E

Suala la michezo mashuleni kupewa kipaumbele likiwemo suala la mchakamchaka

Kusimamia nidhamu za wanafunzi ikiwemo suala la viongozi wa dini kufundisha vipindi vya dini mashuleni ili kuondoa mmomonyoko wa maadili.

Kuweka makambi kwa madarasa ya Mitihani likiwemo suala la usimamizi mzuri wa prepo

Katika kikao hicho zawadi mbalimbali ikiwemo fedha taslim na vyeti vilitolewa kama motisha kwa shule zilizofanya vizuri kwà vigezo mbalimbali vya kielimu kwa elimu ya Msingi na Sekondari.

# Mafunzo ugawaji wa Neti Mashuleni



Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imefanya mafunzo ya mfumo kwa ajili ya mradi wa ugawaji wa neti kwa shule za Msingi kwa Maafisa Elimu Kata na Walimu wakuu yamefanyika leo Februari 16, 2023. Mafunzo yamefanyika kwenye ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri.

Mfumo utakaotumika katika ugawqji wa Neti ni wa SIS ( School Information System).

Neti hizo zinatarajiwa kugawiwa mashuleni kwa wanafunzi hivi karibuni. Kupitia mradi huu Halmashauri itaweza kupunguza tatizo la ugonjwa wa Malaria.

# Mkuu Mkoa Akagua Miradi Chanwino



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule , amemshukuru Rais wa M

Jamhuri ya Muungano wa Tanznaia , Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia shilingi takribani billion 12 za ujenzi wa bwawa la maji kwaajili ya kilimo cha umwagiliaji, mradi unaotekelezwa katika kata ya membe iliyopo wilaya ya Chamwino.

Ameyasema hayo wakati wa ziara ya kukagua mradi huo 01, februari 2023, amesema mradi huo ukikamilika utapunguza kilimo cha kutegemea mvua nakuanza kilimo cha umwagiliaji.

Mhe Rosemary alisema kilimo cha uhakika ni cha kisasa ili mazao yasikose maji baadaya mvua kukata.

“Mhe. Rais ameziweka kwasababu anajuwa kuwa wanachamwino wanahitaji kilimo mmekuwa ni wakulima wa siku nyingi na mmekuwa mkilima kilimo cha kutegemea mvua”.

“Uhakika wa kilimo cha kisasa ni cha umwagiliaji mvua inaisha unaendelea kumwagilia kwa hiyo mazao hayakosi maji hiyo ndio dhamira ya Mhe. Rais hataki tena kusikia Chamwino ina njaa,” Alisema Mkuu wa mkoa.

Hata hivyo amewataka wanachi kuhakikisha wanaulinda mradi huo na kukamilika kwa uhakika ili kutekeleza malengo yaliyokusudiwa kupitia mradi huo

Mkuu wa mkoa alisema fedha zinatolewa n Mhe. Rais kupitia Serikali kuu kwaajili ya utekelezaji wa miradi zifanyiwe kazi kwa wakati na kwa ubora ili wananchi waweze kupata huduma iliyokusudiwa.

Aidha amewataka wakandarasi kuwa makini katika utelekezaji wa miradi wanayopewa na Serikali, pia amewata mainjinia kuwepo eneo la mradi ili kuhakikisha utekuelezaji ukamilika kwa ubora unatakiwa.

“Lakini nisisitize sana leo tumepewa sisi wakandarasi wazawa wa kitanzania ni kwa upendo wa Mhe Rais kwa hiyo fanyeni kwa uhakika, mabwawa haya hayataki wizi yanataka umakini mkubwa bila kuruka hata hatua “.

“Wananchi kuweni walinzi wa kwanza katika huu mradi lakini dhamira ya Mhe. Rais wetu na Serikali fedha zikitolewa, miradi ifanyike kwa wakati na kwa ubora ili wananchi waende kupata huduma waliyoikusudia,”alisema.

# Chamwino Yapongezwa Ukusanyaji Wa Mapato

Waheashimiwa Madiwani wameipongeza menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino na viongozi wote kwa jitihada wanazofanya katika kukusahya mapato ambapo mpaka kufikia mwezi desemba 2022 tayari wamekusanya asilimia 62 na kuwa ya kwanza kimkoa.

Hayo yameelezwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya pili kilichofanyika Januari 27, 2023.

Katika kikao hicho pia Mkuu wa Wilaya ya Chamwino Mhe. Gift Isaya Msuya alipokuwa akitoa Salamu za Serikali amezipongeza Idara za Ardhi, Elimu hususani Elimu Msingi, fedha na Afya kwa kufanya vizuri kwenye Idara zao.

Vilevile amezitaka Idara nyingine kujitatimini na kuiga mfano huo kwenye Idara zao, na yeye mwenyewe atakuwa nazo bega kwa bega kuhakikisha zinafanya vizuri.

Mkuu wa Wilaya pia ametumia nafasi hiyo kuelekeza viongozi wote kuhakikisha wanakwenda kushughulikia suala la wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao bado hawajalipoti shuleni wanakwenda shule hata kama hawatakuwa na sare za shule. Wazazi waendelee kushughulikia sare za shule watoto wakiwa shuleni

Wahe. Madiwani walimpongeza Mkuu wa Wilaya kwa kuendelea kuaminiwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika nafasi yake hiyo na hivyo kuendelea kuitumikia Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino.



# Chamwino Yaweka Mikakati Kupandisha Ufaulu Elimu ya Msingi



Mkuu wa Wilaya ya Chamwino Mhe. Gift Isaya Msuya amefanya kikao kazi na walimu wakuu na Maafisa Elimu Kata leo Januari 19, 2023 chenye lengo la kuweka mikakati itakayowezesha Wilaya kufanya vizuri kitaaluma kwenye elimu ya msingi.

Kikao hicho kimefanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ambapo alipokuwa akifungua kikao amepongeza juhudi zilizofanyika mwaka jana kwa kuendelea kulinda nafasi waliyokuwa nayo pamoja na kuongeza ufaulu kwa asilimia 0.8.

Mkuu wa Wilaya pia ametumia kikao hicho kutoa maelekezo mbalimbali yakiwemo masuala ya uandikishaji wa wanafunzi wa awali na darasa la kwanza ambao wanaonekana kurandaranda kwenye maeneo ya biashara na kilimo wafuatiliwe na kuchukua hatua ili waende shule. Aliendelea kusema kuwa walau kufikia mwezi wa pili wafikie asilimia 100 au ikipunguwa sana iwe asikimia 90.

Vilevile aliongelea kuhusu maadili ambapo kumekuwa na masuala ya ulawiti kwa wanafunzi, walimu na wanafunzi kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi kwa wanafunzi kulawitiana. Alieleza wazazi wanaamini malezi ya watoto wao yanatoka kwa walimu.

Alisisitiza pia suala la utoaji wa chakula cha mchana shuleni ambapo bado liko chini. Aidha alizungumzia suala la maelekezo ya mkoa kuhusu upandaji wa miti ambapo alwataka walimu kuwasimamia wanafunzi kila mmoja apande mti na kuusimamia hadi utakapokuwa na akimaliza shule walisishwe wanaobaki.



Vilevile alielekeza kila shule na kila kata ianzishe vitalu vya miti na miche hiyo itakapokuwa tayari igawiwe kwenye taasis za Serikali ili ipandwe na kila kaya pia itapaswa kuapanda miti mitano na kuanzia mwezi wa tatu watapita kukagua.

Suala la shule kuwa chafu, alielekeza walimu wawasimamie wanafunzi kufanya usafi.

Suala la kusaini mikataba alieleza kuwa mkataba ni sheria hivyo kwa kushindwa kutekeleza yaliyomo kwenye mkataba watachukuliwa hatua. Aliendelea kueleza kuwa mitihani ya kila mwezi ndio itakayotumika kupima matokeo( performance appraisal) watakaofanya vizuri watapongezwa na watakaofanya vibaya watapewa bendera nyekundu wakapeperushe kwenye shule zao.

Aliwaomba wawe tayari kujifunza na kufanya mabadiliko. Vilevile wawe na utayari wa kupokea maelekezo ya viongozi. Wajifunze kwa wengine waliofanikiwa hawataonekana wajinga kwa kufanya hivyo.

Mkuu wa wilaya pia aliahidi kusimamia haki za walimu na watumishi wengine kama waziri wa TAMISEMI alivyoelekeza lakini alisisitiza haki iendane na wajibu.

Katika kikao hicho wajumbe walipitia na kujadili kuhusu mpango kazi wa Mkoa kuhusu elimu ya msingi pamoja na mpango mkakati maalum wa Wilaya kwa ajili ya darasa la saba.

# Chamwino Yaweka Mikakati Utatuzi wa Changamoto za Mazingira



Mkuu wa Wilaya ya Chamwino Mhe. Gift Isaya Msuya amefanya kikao na wadau wa mazingira Wilayani chamwino pamoja na viongozi mbalimbali ngazi ya Wilaya, Kata na vijiji wakiwemo Waheshimiwa Madiwani.

Kikao kimefanyika January 10, 2023 kwenye ukumbi wa Halmashauri. Lengo la kikao hicho ni kujadili na kuweka mikakati mbalimbàli ya kutatua changamoto za mazingira zinazoikabili Halmashauri ya Wilaya ya chamwino.

Katika kikao hicho Mhe. Mkuu wa Wilaya alitoa maelekezo mbalimbali yakiwemo masuala ya kupanda miti ambayo ni maelekezo ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira ya kupanda miti ml. 1.5 kila mwaka kwa kila Wilaya.

Na miti hii inapaswa kuoteshwa na wadau mbalimbali mazingira kwa kuanzisha vitalu vyao.

"Na hii huko Tabora nilikotoka tulikuwa na utaratibu kila kata ilikuwa na utaratibu wa kuanzisha kitalu mahali kwenye Taasis ya Serikali au kwenye chanzo cha maji na wanapangiwa idadi ya miche



wanayotakiwa kupanda na kuistawisha". Alisema Mkuu wa Wilaya. Kazi ya mazingira ni kuwatafutia mbegu na kuwapa utaalam wa namna ya kuotesha na kuitunza miche ya mbegu iliyooteshwa ili kupata miche itakayowasaidià kupanda kwenye kata husika. Maelekezo yalitolewa Mkurugenzi ahakikishe kufikia mwezi machi, 2023 kila kata iwe imeshapanda vitalu vya miti.

"Natoa wito kufikia mwezi wa tatu kila kata ianzishe kitalu cha miti, ikiwemo ya kivuli na ya matunda na itagawanywa kwa muijbu wa maelekezo yaliyotolewa. Alisema Mkuu wa Wilaya.

Kila kata igawiwe idadi ya miche ya kupanda kutokana na idadi ya miti waliyopangiwa kupanda kati ya miche Ml. 1.5 iliyopangiwa Wilaya na watapita kukagua. Vivyo hivyo mgawanyo ufanyike kwa kila kata kwa miche itakayotolewa na TFS na tuhakikishe miti hiyo inatunzwa, kumwagiliwa na inakuwa.

Pia maelekezo ya Mkuu wa mkoa wa Dododoma kupitia kampeni ya upandaji miti kila kaya inapaswa kupanda miche mitano, miwili ya matunda na mitatu ya kivuli na atafanya ukaguzi kila Wilaya.

Aliomba wadau wa madini ya ujenzi, wakandarasi waliopewa kazi za ujenzi wa barabara maji na  wapenzi wa mazingira, shulè na vituo vya afya  aliwaomba washirikiane kwa pamoja maana bajeti ya Kitengo cha mazingira ni ndogo sana.

Katika kikao hicho wajumbe walijadili na kuweka maadhimio mbali mbali ambayo wadau wote wa mazingira, viongozi wa kata, vijiji, vitongoji na ngazi ya Wilaya watapaswa kuyatekeleza yanayohusu mazingira hususani usafi na upandaji wa miti

Chamwino Buigiri

Chamwino Dc

Chamwino_dc

www.chamwinodc.go.tz

S.L.P 1126 Dodoma